## Kusoma Zaidi

## Katika msingi ya hatua za uandishi tunazingatia hatua hizi ili kukuza stadi ya kuandika kwa utaratibu ufaao.

***i) Maumbo ya herufi:*** Haya ni maandishi ya kimsingi ya herufi kabla ya kuandika ruwaza za herufi. Hizi ni herufi za lugha ambazo mwanafunzi huziandika katika shughuli za kujifunza uandishi katika lugha yoyote.

Kwa mfano: a ,b, m, nd

*ii)* ***kuchora ruwaza***: Hii ni hatua ambayo mwanafunzi hujifunza kuandika herufi kwa kurudiarudia herufi fulani/moja. Mwanafunzi hufanya mazoezi ya kuandika ili aweze kuwa na uwezo wa kuthibiti kalamu anapoandika.

# Ruwaza ya herufi

a → a a a a a a a a a a a a

b → b b b b b b b b b b b b

m → m m m m m m m m m m

***iii) Silabi:*** Umbo la neno linalotokana na kuunganisha herufi moja au zaidi na nyingine. Inaweza kuwa silabi ya herufi moja ambayo mwanafunzi anapaswa kuandika. Kwa mfano;

***ba, me, do, mbi, chu, …***

***iv) Neno:*** Baada ya mwanafunzi kujifunza kuandika au kuchora ruwaza, anasonga hatua ya kuunganisha herufi ili kuunda neno kwa kuzingatia uandishi wa herufi kwa njia kamilifu. Kwa mfano;

***mama, baba, kaka,***

*iv)* ***Hati:*** Maneno yanayoandikwa yanapaswa kuzingatia hati nadhifu, kamili, inayoonekana na kusomeka vizuri.

## Kusoma Zaidi

***v) Mafungu:*** Baada ya kuweza kuandika maneno mwanafunzi anapaswa kuandika mafungu ya maneno. Mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa kuandika maneno kadhaa kikamilifu na kwa hati nadhifu. Kwa mfano;

***mama yangu***
***kalamu yangu***
***kitabu chake***

***vi) Imla:*** Kuandika imla kwa mwanafunzi inapaswa kuwa baada ya mwanafunzi kupata uwezo wa kuthibiti kalamu na kuandika kwa hati nadhifu. Imla humfanya mwanafunzi kufanya mazoezi ya kuandika. Kuandika imla kwa watoto wa viwango vya chini unaanza kwa kuandika maneno mafupi na kisha vifungu kwa jinsi anavyokua.